## UTAGULIZI

## Kosmolojia ya Martinus – mtazamo wa matumaini katika maisha

### Jitambue

Jinsi ambavyo maisha yetu yalivyo kitendawili, halikadhalika ndivyo siri ya ulimwengu itakavyobaki kuwa kitendawili kwetu sisi. Kwa maana Kosmolojia, ambayo inaelezea uhai katika mapana yake yote, inahusu sisi wenyewe pamoja na yale yote ambayo ni muhimu kwa maisha yetu. Kaulimbiu ya mtazamo wa duniani ni "Jitambue, nawe utauelewa ulimwengu."

### Ulimwengu ni kiumbe chenye uzima

Fikra kuu katika mtazamo wa Martinus ni kuwa ulimwengu una uhai na akili. Ulimwengu ni kiumbehai mmoja anayejumuisha viumbe na vitu vyote. Kiumbehai hiki ni uzima wa mfungamano wa viumbe na vitu vyote ulimwenguni ambavyo vinadumu na kujiendesha kama kitu kimoja kikuu. Katika dini, kitu hiki kikuu kinajulikana kwa neno "Mungu". Hivyo, uzima haugawiki. Katika kanuni za mahusiano, uwezo wa kuishi kwa maelewano mazuri na kila mtu utaendelea kukua. Hatimaye tutazidi kuuelewa mfungamano huu na kuishi kama "kitu kimoja chenye uzima". Hivyo tutatimiza kanuni za uzima, na kumpenda jirani kama tunavyojipenda sisi wenyewe.

### Siyo dini, wala uanachama

Kosmolojia ya Martinus siyo dini. Aidha hakuna uanachama kwa mtu yeyote. Kosmolojia ya Martinus ni maelezo ya mfungamano na kuwepo kwa viumbe na vitu vyote. Kuwa, kila kiumbe na kila kitu ni sehemu katika jamii ya mfungamano wa viumbe na vitu vyote. Martinus hatarajii kupata waumini wa fikra zake. Aidha hana nia ya kubadilisha watu ili wajenge imani katika maandiko yake. Bali anataka tuchanganue kama kile alichokiandika kina ukweli kulingana na mambo yanayotokea katika maisha yetu.

Martinus halazimishi maadili yoyote ya kufuata, bali anaelezea kuwa maisha yetu ndiyo yatatujengea maadili *ya* hali ya juu katika mioyo na akili zetu. Ameasisi sayansi ya kiroho inayoelekeza misingi ya kuwepo kwa uzima wa milele kwa kufanya michanganuo inayodhihirisha kuwepo kwa

mfungamano katika ulimwengu. (Ukweli ni mkubwa na umesambaa).

**Mtazamo wa uzima**

Katika maandiko yake, Martinus anaanzisha mtazamo mpya wa maisha – mtazamo wa mfungamano wa uzima. Kifo ni mageuko tu katika mfungamano wa ulimwengu, lakini uzima upo milele. Ili tupate kuuelewe, inatubidi tuamini kuwa uzima unadumu milele.

**Mnyama hadi binadamu halisi**

Katika mageuko, inaeleweka kwamba Mtu ni mnyama aliyeendelea na kupitia mabadiliko makubwa sana. Jambo jipya kuhusu mageuko, katika fikra za Martinus, ni kuwa kila mtu ni mshirika binafsi katika mfungamano wa harakati za mageuko. Daima watu ni viumbe walio katika mpito wa mageuko; ni nusu-mnyama, nusu-binadamu. Mwelekeo wa ubinafsi wetu unatokana na mapambano magumu ya maisha katika jamii ya wanyama, kwa kuwa ni jambo la muhimu na lenye manufaa kwao. Lakini asili hii ya kinyama haifai wakati huu tulionao, kwa kuwa inahatarisha maisha ya watu. Katika mageuko haya, ubinafsi, umekuwa tabia ambayo inayaongoza matendo yetu kuelekea kwenye malengo ya kujali manufaa ya kiubinafsi, bila sisi wenyewe kugundua. Ndani ya mioyo yetu upo mvutano kati ya akili yetu ya kinyama ya awali, na kuzaliwa kwa mwamko mpya wa kiutu. Hatima ya mfungamano wetu ni kuwa raia katika jamii halisi ya watu. Misingi ya maisha katika jamii hii ni kutokuwa na ubinafsi na *ustawi wa* ujirani mwema wenye upendo kati ya mtu na mwenzake.

**Hatima yetu iko mikononi mwetu**

Ni kwa nini watu wanapata matatizo mengi? *Kwa nini kuna majanga mengi yanayotupata ambayo kwayo hatuwezi kulaumiwa kwamba tumeyasababisha sisi?* Bila kuuelewa ukweli kuhusu milele, hatuwezi *kubaini* viini vya matatizo yetu. Hatuelewi kuwa maisha yetu ya kimwili ya sasa ni kiungo tu katika mpango mkuu – kwa hakika, ni utaratibu wa mageuko unaoendelea milele na milele. Hivyo hatujui kwamba maisha yetu ya sasa yanatokana na akili na tabia zetu. Halikadhalika, tunatambua kwamba mawazo na matendo yetu ya sasa yanajenga mfumo ambao hatimaye utatukuta katika uhai wetu wa baadaye.

Martinus anachanganua mpangilio wa milele kuhusu uzima. Anasema hakuna kifo. Kuna vifaa na viumbe, ambavyo daima vinafanyiwa matengenezo, vinaundwa na vinaharibika; lakini kiini chake - yaani uzima = unadumu milele.

Kuna vifaa vya kimwili na vya kiroho. Tunaishi katika dunia mbili; ya kimwili na ya kiroho. Lakini tunaitambua dunia ya kimwili pekee. Kwa hiyo hatima yetu ni siri. Kulingana na Martinus, tunajitengenezea hatima yetu. Mwamuzi wa hatima yetu ni fikra na matendo yetu wenyewe. Hatima yetu, yaani maisha yetu ya baadaye, iko mikononi mwetu. Ndani ya nafsi zetu upo uwezo uliolala ambao hatujautumia ambao unasubiri tuutumie.

**Sababu ya matatizo**

Je, matatizo ya duniani yana kusudi lolote? Ndiyo. Kulingana na Martinus, tatizo lina jukumu. Linatubadilisha hatua kwa hatua na kujenga nafasi ya huruma na ubinadamu katika nafsi zetu. Matatizo ni matokeo ya desturi ya kuishi kinyama, "Kila mtu nafsi yake". Kumletea mwenzio baa ni kudhihirisha kutoijuwa kanuni ya hatima: "Kila mtu atavuna kile alichopanda". Ijapokuwa hatujuwi tulitendalo, tunajifunza kutofautisha kati ya mema na maovu, kwa sababu tunajuwa kwamba tutavuna tulichopanda! Tutakapofikia hapo tutatambua kuwa kufanya yaliyo mema ndiyo njia pekee ya kudhihirisha utu wetu.

**Je, kuna haki katika uzima?**

Ni muhimu tuamini kuwa katika uzima, *daima* haki inatendeka. Mfumo wa mahakama katika jamii yetu unazidi kuelekea kwenye haki kuu. Martinus anasema, utaratibu uliopo kwenye ulimwengu wenyewe ni dhamana ya kuhakikisha kuwepo kwa kanuni za milele za uzima pamoja na haki, katika hali na matukio yote ya uzima. Kwa vile tutapatwa na lile linalotokana na matendo yetu, hivyo hakuna anayepata tatizo kwa maonevu. Sababu ya matatizo yetu hayatokani na wale tunaowadhania kuwa ni maadui wetu. Hawa ni vifaa tu vinavyojibu matokeo ya matendo yetu yaliyopita, au matendo ya vizazi vilivyotutangulia. "Kitovu cha maovu yote" kimo ndani ya nafsi zetu. Mtu bado hajuwi kuwa adui yake mkubwa ni yeye mwenyewe, asema Martinus. Kwa kuwa hatuwezi kupata matatizo, isipokuwa yale tunayowaletea wengine, tunaanza kupata hisia kuwa ipo haki kuu zaidi katika kila jambo.

**Tarajio kuu la watu wote**

Mageuko yote yana misingi mipana na kanuni za mfungamano. Uelewa wa kanuni hizi muhimu za mfungamano huu mpana unatuwezesha kubaini lengo kuu la baadaye kwa binadamu. Kama jinsi ilivyo kawaida kwa mchana na usiku, na masika na kiangazi, hivyo ndivyo werevu unavyoambatana

na ujinga, na upendo nao kuambatana na chuki. Lengo la mageuko katika mfungamano wa ulimwengu kwa dunia hii ni ufalme wenye amani duniani. *Mageuko ni matokeo ya kuwepo kwa muungano wa mataifa ya dunia na kuanzishwa kwa mfumo wa kimataifa wa mahakama. Katika Kosmolojia yake, Martinus anachanganua mahitaji muhimu ya hatua za kufikia taifa moja, dunia moja.

Hata hivyo, taifa moja kwa dunia nzima haitafikiwa kwa ubabe, bali kwa kwa njia ya mageuko pekee. Katika sura ya mfungamano wa ulimwengu ambao una mchanganuo wenye mantiki, Martinus anatuonesha kwamba upendo kwa jirani zetu hapa duniani ni matokeo ya kanuni za utaratibu uliopo ulimwenguni. Ujirani na ushirikiano mwema na jirani ni mchanganyiko wa manufaa unaotokana na busara na huruma. Hii ni hali ya akili ambayo inakubalika kuleta upendo, jambo ambalo ni la msingi katika ulimwengu.

**Martinus alikuwa nani/mtu gani?**

Martinus alikuwa ni mwandishi toka nchi ya Denmaki. Maandishi yake mbalimbali yamechapishwa katika kitabu kinachoitwa "Agano la Tatu". Kitabu chake kikuu ni Livets Bog (Kitabu cha Uzima) katika Lugha ya Kidenmaki. Ameandika nyongeza yake (katika vitabu 4), inayoitwa "Sura ya Ulimwengu wa Milele" ("The Eternal World Picture" kwa Kiingereza). Nyongeza hii ina alama za michoro ya rangi na maelezo yake, na maelezo ya misimamo ya Kosmolojia yake. Aidha ameandika "Logic" (kwa tafsiri ya Kiingereza) ama "Mantiki" (kwa tafsiri ya Kiswahili) ambacho ni utangulizi wa Livets Bog. Aidha ameandika vijitabu takribani 30 hivi.

Martinus alizaliwa mwaka 1890 katika mji mdogo wenye kituo cha garimoshi kaskazini ya Jutland, nchini Denmaki. Aliishi miaka tisini. Machi 1921 ndio mwanzo wa mawazo na maandiko yake ambayo ni matokeo ya mabadiliko makubwa ya hisia. Katika dibaji ya "Livets Bog", Martinus anaandika kuhusu hilo kama ifuatavyo:

> "Ubatizo wa mfungamano, wa moto ambao nimeupitia – ambao mchanganuo wake siwezi kuuelezea kwa undani hapa - ulinipa ukweli kwamba maono mapya kabisa yalikuwa yamenitokea na kunipa uwezo dhahiri wa kuona bayana na kuelewa nguvu zote za kiroho, sababu zilizojificha, kanuni za ulimwengu za milele, nguvu za msingi na taratibu za vitu duniani. Siri ya kuwepo kwa vitu na viumbe haikuwa siri tena kwangu. Nikawa ninaujuwa uzima wa ulimwengu wote, na hivyo "kuingizwa katika taratibu za utukufu wa uumbwaji".

Mabadiliko haya ya kimawazo na mtazamo mpya nilioupata ndiyo chanzo cha kazi ya Martinus kama mwandishi. Aliandika tangu 1921 hadi kifo chake mwaka 1981.

*Rolf Elving (1985)*

Imetafsiriwa na Elliah E.E. Mligite

**Taasisi ya Martinus** iliyoko Frederiksberg, Kopenhagen ilichapisha vitabu vyote vya Martinus hadi mwishoni mwa 1981, baadaye Borgen's Publishers walianza kuvichapisha tena kwa lugha ya Kidenmaki. Taasisi ina nafasi ya kufundishia na utawala, duka la vitabu, madarasa, na huendesha kozi, na mpango wa kujisomea unafanyika kila kiangazi.

The Martinus Institute (Taasisi ya Martinus)
Mariendalsvej 96
DK-2000 Frederiksberg, Denmaki
Simu: +45 3834 6280
Faksi: +45 3834 6180
Baruapepe: institut@martinus.dk

**Kituo cha Martinus**, Klintvej 69, Klint, DK-4500 Nykøbing Sj., Denmaki, kilianzishwa mwaka 1935 pwani ya kaskazini-magharibi ya Sjælland (Zealand) yapata maili 60 kutoka Kopenhagen. Ina uwezo wa kupokea wageni 200 katika ghorofa, vyumba, vibanda vya mbao na kwenye maeneo ya kupiga kambi (mahema) yaliyopo. Kituo kina huduma za jiko katika kila ghorofa na mabanda yote; aidha Taasisi inao mgahawa kwa ajili ya wageni wasiokula nyama (walaji wa mboga). Kwa kawaida wageni wengi wa Kituo ni watu wa kutoka nchi za Skandinavia. Hata hivyo Kituo huendesha kozi ya kimataifa ya majuma mawili kila mwaka kwa watu wanaoongea Kiingereza na Kijerumani. Vilevile upo mpango wa mafunzo kwa watu wasio na asili ya Skandinavia katika vipindi vya Kipupwe na Vuli (yaani vipindi vya mpito vya kutoka Masika kuingia Kiangazi na Kiangazi kuingia Masika. Lugha ya kimataifa ya Kituo ambayo ni Kiesparanto pia hufundishwa kwenye Kituo.